# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI

**24 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI - TAREHE 24 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**662 MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Kituo cha Afya Mkolani.

**663 MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Wanasaikolojia ngazi ya Kata ili kusaidia kukabiliana na tatizo la Afya ya Akili.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**664 MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali haioni haja ya kuwapandisha madaraja ya kiutumishi Madaktari Bingwa bila sharti la ulazima wa kuandika andiko.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**665 MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALLOS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itakomesha kabisa uzalishaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki nchini.

**WIZARA YA AFYA:**

**666 MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, utaratibu upi unatumika kutoa huduma za afya kwa Watu wenye Ulemavu wasio na uwezo kabla ya kuanza kutumika kwa Bima ya Afya kwa Wote.

**WIZARA YA KILIMO:**

**667 MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza Zao la Karanga katika Mkoa wa Dodoma.

**WIZARA YA UJENZI:**

**668 MHESHIMIWA STEPHEN LUJWAHUKA BYABATO (BUKOBA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Busimbe Senta - Kagemu - Kemebose hadi Kyamunene - Bukoba Mjini itajengwa kwa kiwango cha lami.

**669 MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mtwara - Mingoyo - Masasi utaanza ikizingatiwa imeharibika na inachukua mizigo mikubwa ya Makaa ya Mawe.

**670 MHESHIMIWA MICHAEL CONSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kiwango cha lami kutoka Mlandizi hadi Ruvu Stesheni ya SGR.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**671 MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaondoa nyumba zisizo na ubora nchini.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**672 MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali inakabiliana vipi na ongezeko la idadi ya Wazee katika nyanja za afya, lishe na huduma nyingine za msingi.

**WIZARA YA MAJI:**

**673 MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka Miradi mikubwa ya maji kwenye Miji Midogo ya Mlangali, Lugarawa na Luilo ili kuendana na kasi ya ongezeko la watu.

**674 MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji wa Munyu katika Kata ya Irisya Jimbo la Singida Magharibi.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa kwa Hatua zake zote)***

Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2025 *(The Appropriation Bill, 2025).*

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**24 JUNI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA